

Mola nusuru Kenya

Kila paa linavuja, nchi ikiwa na dhiki,
Kila kona ni vioja, Kusini na Mashariki,
Huvunjika madaraja, yavumapo ya ghariki,
Kenya tunaangamia, Jalali tupe nusura.

Baringo wanafa watu, kwa mabomu na bunduki,
Wauana wana wetu, kama kulivyo Iraki,
Ni milio ya mitutu, nao watu kifariki,
Kenya tunaangamia, Jalali tupe nusura.

Njaa nayo jinamizi, kila pembe ni mateso,
Wanafunzi kwa wazazi, tuna njaa kwenye nyuso,
Tana River na Kibwezi, Turkana pia Teso,
Kenya tunaangamia, Jalali tupe nusura.

Utapiamulo jama, kwa vikembe meshamiri,
Kwa kukosa cha kuchuma, wamebaki mafakhiri,
Njaa kali yawauma, hawana kujisetiri,
Kenya tunaangamia, Jalali tupe nusura.

*Ramadhan Abdallah Savonge
"Malenga wa Nchi Kavu",
Chuo Kikuu SEKU, Kitui*